

HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI



TANGAZO ! TANGAZO! TANGAZO! 21/04/2017

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI, ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE WILAYANI MISUNGWI, KUHUSU ZOEZI MAALUM (OPERATION) YA MALIPO YA ADA YA VIBALI VYA UJENZI KWA WANANCHI WOTE WALIOJENGA BILA KULIPIA KIBALI CHA UJENZI KUTOKA IDARA YA UJENZI .

KIBALI CHA UJENZI KINATOLEWA KWA KILA MWANANCHI ANAYEJENGA NYUMBA KATIKA MAENEO YA KIWANJA KILICHOPIMWA NA AMBACHO HAKIJAPIMWA ,NA MALIPO YA KIBALI CHA UJENZI YANAFANYIKA KWA MUJIBU WA SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI ZA MWAKA 2014,GN/198/2001 ILIYOTANGAZWA NA GAZETI LA SERIKALI NA.54 LA TAREHE 20/02/2015 INAYOMTAKA MWANANCHI KULIPIA ADA YA KIBALI CHA UJENZI KWA VIWANGO VIFUATAVYO:-

1. MAJENGO YA KAWAIDA KUENZIA Tsh,30,000/= HADI 50,000/=
2. MAJENGO MAKUBWA ,KUENZIA Tsh, 60,000/= HADI 100,000/=

VILE VILE MALIPO YA ADA HII YANAFANYIKA KULINGANA NA VIWANGO VYA UKUBWA WA MITA ZA MRABA ZA MAENEO YA KIWANJA CHA MHUSIKA.

HIVYO,WANANCHI WOTE MNAOMBWA KULIPIA KIBALI CHA UJENZI WA JENGO/MAJENGO MAPEMA KABLA YA TAREHE 30, MEI 2017, VINGINEVYO UTATOZWA FAINI NA HATUA ZA KISHERIA ZITACHUKULIWA DHIDI YAKO KWA KUKAIDI NA KUKATAA KUTEKELEZA SHERIA ZA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA.

IMETOLEWA NA:

ELIURD MWAITELEKE
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MISUNGWI